

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
30 Agosti 2008**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Ally Mzee Amiri
Bashiri Rashidi
Beda John Mkusu
Dominata Rwechungura
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frank Peter Rwechungura
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Mitanga
Mohamedi Saidi
Mussa Alex
Nickson Kilunga
Paulo Atibu Hatibu
Pendo January
Shamte J Kigoma

Wageni

Corporal Abuu Mwakipesile Traffic Police
Sergeant Dumu Mwahigenge Traffic Police
Engineer George Daffa TANROADS

Mkutano huu ulikuwa mkutano maalum wa UWABA pamoja na wageni rasmi kuhusu mpango wa kuandaa kongamano la kila mwezi kuhusu masuala ya usafiri wa siyo ya moto Dar es Salaam. Engineer George Daffa na Corporal Abuu Mwakipesile walikuwa kwenye mafunzo ya wakufunzi ya usalama wa baisikeli basi wameshawahi kushirikiana na UWABA.

Tuliwakaribisha wageni kutoka TANROADS na traffic police na tuliwashukuru kwa kuhudhuria mkutano. Tuliongea kuhusu historia ya wazo la kongamano. Wazo tulipata kutoka Andrew Wheeldon wa BEN South Africa, ambaye alisaidia kuandaa kongamano jiji la Cape Town, South Africa. Malengo ya kongamano yalikuwa kuleta pamoja mashirika mbali mbali ya serekali pamoja na mashirika ya siyo ya kiserekali ili kushirikiana kufika lengo la jiji nzuri na salama kwa wapanda baisikeli na watembea kwa miguu.

UWABA tuliomba ushauri kutoka wageni wa serekali kuhusu vipi tunaweza kuandaa kongamano kama hili. Wageni walipendekeza kwamba serekali ya jiji ni muhimu sana katika kitu kama hiki. Tuliwaalika kwenye mkutano huu (idara ya mabasi ya haraka DART na pia halmashauri la jiji) lakini hakuna mwakilishi aliyehudhuria. Wageni pia walipendekeza kwamba tutafute fedha ili kulipia gharama za mikutano ya kongamano. Wageni pia walisema kwamba wao wenyewe waunga mkono na kongamano lakini ni

nzuri tuwe na wakubwa katika serekali ambao wanaunga mkono pia ili kongamano ifike malengo yake kama wabunge wa Dar es Salaam, diwani ya halmashauri za manispaa na wameya. Mtu au watu hawa wanaweza kusaidia kongamano lijulikane na kazi yake ifanyikiwe na itasaidia kupata sehemu ya mikutano.

UWABA tulisema tutafuatalia na serekali ya jiji, wabunge, madiwani na wameya ili kupata mkubwa kutusaidia na kutushauri vipi kuandaa kongamano.

Tuliongea kuhusu jina la kongamano na tuliamua “Kongamano la Usalama wa Wapanda Baisikeli na Watembea kwa Miguu Dar es Salaam” au kwa mfupi KOBAMI-Dar.

Baada ya hapo UWABA tuliuliza kuhusu masuala mbali mbali yanayohusika TANROADS na traffic police.

Kuhusu suala la barabara za Sam Nujoma na Kilwa, UWABA tulieleza kwamba tumeandika barua mbili na tumepata majibu mawili, lakini tuliandika barua ya tatu ambayo bado hatujapata jibu. Barua inaeleza tumeonaje barabara zilivyojengwa mpaka sasa na inauliza njia za baisikeli ni wapi sawa sawa kwenye barabara hizi.

Kuhusu barabara ya Morogoro, UWABA tulionyesha barua tuliyotumia serekali ya jiji, na jibu tulilopata, lakini barua kutoka halmashauri haijajibu vizuri maswali yetu kila moja, hasa kuhusu wazi wazi kwamba magari yataingia njia za baisikeli.

Tuliuliza kuhusu tangazo la juzi juzi kwamba daraja itajengwa Kigamboni, na kama itakuwa na njia za baisikeli. Engineer Daffa alisema kwamba inajengwa na National Social Security Fund (NSSF) na siyo serekali yenyewe. UWABA tulisema kwamba tutaandika barua kwa NSSF kuhusu hiyo.

UWABA tuliongea kuhusu umuhimu wa matuta na zebra ambazo pia ni tuta kwenye maeneo kama Kigamboni na Tandale. UWABA tulimwazima Engineer Daffa kitabu tulichopata kutoka Professor Rwebangira ambacho kina taarifa nyingi kuhusu “traffic calming measures”.

UWABA pia tuliongea kuhusu matatizo ya mashimo kubwa kama lile kariba na Kagera, Morogoro Road, upande wa kushoto unapoelekea mjini, ambapo inaonekana watu wa maji au umeme walifanya shimo. Engineer Daffa alisema kwamba ni ujibu wa kampuni ya maji au umeme kurekebisha mashimo yanayofanya barabarani. Pia tuliongea kuhusu shida la alama za barabara kuibiwa, na vipi kuziweka sawa na zege.

UWABA tuliuliza traffic police kuhusu shida ya service roads. Walisema kwamba Kamishna Suleiman Kovu juzi juzi ameanzisha operation kupiga faini ya magari yanayopaki kwenye service roads. UWABA tulisema tutaandika barua ya pongezi ya operation hiyo, na tunashauri kwamba itangazwe kwenye vyombo vya habari ili watu wajue.

UWABA tulisema tuliandika barua kwa traffic police kuuliza kama kuna sheria au tangazo lolote la serekali linaloeleza matumizi ya service roads. Wageni walisema watafuatalia jibu na taarifa hii.

UWABA tulisema kwamba tulipata kijitabu na namba za simu za traffic police zinazotangazwa ili kutoa repoti ya makosa, lakini wanachama walipojaribu hakuna jibu au simu hazipatikani. Watu wa traffic police walisema kwamba labda ni simu za zamani na watafuatalia kupata namba za sasa.